# NAMNA TAMTHILIA INAVYOWEZA KUTUMIWA KUFUNDISHA USHAIRI KATIKA SHULE ZA UPILI: UCHUNGUZI KIFANI WA KAUNTI NDOGO YA TESO KASKAZINI, BUSIA KENYA

**Hillary Mauka Mukoya, Misiko Wasike, Edwin Masinde na Deborah Nanyama Amukowa**

# 1.0 Utangulizi

- Makala haya yanahusu namna tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha ushairi katika shule za upili nchini Kenya
- Tamthilia na ushairi ni tanzu za fasihi ambazo zinafundishwa na kutahiniwa katika shule za upili katika karatasi ya tatu (102/3) nchini Kenya.
- Tamthilia ni utungo ulioandikwa au usioandikwa ambao unalieleza na kuliweka wazo linalotendeka mbele ya hadhira na ni moja kati ya tanzu kubwa na muhimu za fasihi na si rahisi kuonyesha tofauti zilizopo kati ya tamthilia na tanzu nyingine za fasihi kwa sababu tanzu hizi huingiliana.
- Ushairi ni sanaa ya lugha ambayo inaeleza wazo kwa njia ya mkato na kwa namna inayoteka hisia za msomaji au msikilizaji; ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi.

# 1.2 Suala la Utafiti

- Taasisi ya Elimu ya Kenya inapendekeza kuwa mbinu ya mwelekeo mseto itumike katika ufundishaji wa somo la Kiswahili mathalani masomo ya lugha na fasihi yafundishwe kwa pamoja ili wanafunzi wayachangamkie. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu utanzu mmoja kutumika kuwasilisha mawazo katika utanzu mwingine, hivyo basi mwelekeo mseto umezingatiwa. Japo mbinu ya mwelekeo mseto imezingatiwa pakubwa na wataalam mbalimbali, pana haja ya kufanya utafiti kuhusu namna tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha ushairi katika shule za upili nchini Kenya.

# 1.3 Malengo ya Utafiti

## 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

- Utafiti huu ulichunguza namna tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha ushairi katika shule za upili nchini Kenya.

## 1.3.2 Malengo Mahususi

- Utafiti ulilenga;
- Kueleza namna tamthilia inavyotumiwa kufundisha mtindo katika ushairi.
- Kubainisha matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa muundo wa ushairi.
- Kuonyesha namna tamthilia inavyotumiwa kufundisha maudhui katika ushairi.

# 1.3.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo;

- Ni kwa namna gani tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha mtindo katika ushairi?
- Tamthilia inatumika vipi kufundisha muundo wa ushairi?
- Je, maudhui katika ushairi yanafundishwa vipi kwa kutumia tamthilia?

# 1.4 Umuhimu wa Utafiti

- Utafiti huu utawasaidia walimu wa shule za upili kuboresha zaidi ufundishaji wa ushairi.
- Utafiti huu utatoa mwelekeo mpya katika ufundishaji wa ushairi.
- Ni utafiti utakaozua mbinu ya ziada katika ufundishaji wa ushairi.
- Ni utafiti ambao utatoa mchango katika taaluma ya elimu na lugha kwa kuongezea mbinu moja zaidi ya kufundisha.
- Ni utafiti ambao utakuwa wa manufaa kwa asasi zinazowaandaa walimu kwa kuwa utachangia katika kuboresha zaidi maandalizi yao kuhusu mwelekeo mseto wa ufundishaji wa fasihi.
- Utafiti huu utawafaa waandishi kwa kuwa utawaongezea mbinu zaidi ya kufundishia ushairi.
- Utafiti huu utazua ilhamu ya wanafunzi ya kuchangamkia ushairi kwa kuwa ufundishaji wa tanzu mbili za fasihi utatendeka kwa pamoja na hivyo basi kuwa na ujifunzaji bora wa ushairi.

# 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

- Kiswahili ni somo la lazima katika shule za upili nchini Kenya.
- Wizara ya Elimu ya Kenya inapendekeza matumizi ya mbinu ya mwelekeo mseto katika ufundishaji wa somo la Kiswahili.
- Matumizi ya utanzu mmoja kufundisha utanzu mwingine ni miongoni mwa mbinu ibuka za kufundisha ambazo zinachangamkiwa katika shule za upili.
- Pana haja ya kutafiti mbinu zaidi za kufundishia ushairi ili kuboresha zaidi ufundishaji miongoni mwa walimu.

# 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

- Utafiti huu ulizingatia sifa za tamthilia katika ufundishaji wa ushairi. Sifa hizo ni mtindo, muundo na maudhui.
- Utafiti huu ulilenga kueleza namna tamthilia inavyotumika kufundisha mtindo katika ushairi, kubainisha matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa muundo wa ushairi na kuonyesha namna tamthilia inavyotumika kufundisha maudhui katika ushairi.
- Utafiti huu ulijikita katika mihimili mitatu ya nadharia ya utanzu ambayo ni: tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia na watu hupata msisimko zaidi kunapotumika utanzu mwingine ambao umejaa burudani.
- Tamthilia zilizotumiwa katika utafiti huu ni: Kifo Kisimani (Mberia 2001), Mstahiki Meya (Arege 2009) na Kigogo *(*Kea 2016).

# 1.7 Misingi ya Kinadharia

- Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utanzu. iliyoaosisiwa na Boas (1940).
- Nadharia hii ilitumiwa katika anthropolojia wakati wa Boas katika kuchunguza lugha asilia ya Marekani. Nadharia ya utanzu ni kama kundi, aina, namna au mtindo wa utendaji wenye kuwasiliana ambao huelezwa, huainishwa na kujulikana kuwa ni mali ya kundi husika. Nadharia ya utanzu katika kipindi cha urasimi ililenga kuwekea tanzu mipaka. Hii ni tofauti na nadharia ya kipindi hiki ambayo mara nyingi inaelezea tanzu zilizopo na sifa zao bila kuziwekea sheria zozote na mipaka yoyote.
- Nadharia hii ina mihimili ifuatayo:Tanzu nyingi zinapotumika katika matini fulani huchangia pakubwa kueleweka kwa maudhui.
- Matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia.
- Watu hupata msisimko zaidi kunapotumika utanzu mwingine ambao umejaa burudani.

# 2.0 Mbinu za Utafiti

- **2.1 Muundo wa Utafiti.**
- Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo. Utafiti wa kimaelezo ni utafiti ambao hulenga kueleza hali ya jambo jinsi lilivyo.
- Utafiti huu ulieleza namna tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha mtindo katika ushairi.
- Vilevile ulibainisha matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa muundo wa ushairi.
- Utafiti huu pia ulionyesha namna tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha maudhui katika ushairi.

# 2.2 Eneo la Utafiti

- Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini, Kaunti ya Busia, nchini Kenya.
- Kaunti Ndogo hii ina jumla ya shule thelathini (30) ambazo zimegawika katika shule za wavulana, shule za wasichana na shule za mseto. Eneo hili lina shule moja ya wavulana, shule nne za wasichana na shule ishirini na tano (25) za mseto.
- Eneo hili lilichaguliwa kwa sababu ni miongoni mwa maeneo yanayofundisha fasihi ya Kiswahili na watafitiwa walipatikana kwa urahisi na kwa muda mfupi, hivyo basi watafitiwa walifanikisha shughuli ya kupata data za kutosha kuhusu namna tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha ushairi.

# 2.3 Usampulishaji

- Utafiti huu ulitumia mbinu ya utabakishaji. Shule zilizoshiriki katika utafiti ziliteuliwa kwa kutumia usampulishaji wa kitabaka kwa matabaka yafuatayo: shule za wavulana, shule za wasichana na shule za mseto.
- Sampuli ya kimakusudi ilitumiwa kuteua walimu kwa sababu hao ndio walio na mamlaka ya kufundisha. Walimu wanaofundisha kidato cha tatu ndio waliolengwa katika utafiti huu. Utafiti huu ulimlenga mwalimu mmoja katika kila shule zilizoteuliwa.
- Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini ina shule thelathini (30), hivyo basi asilimia thelathini (30%) ilizingatiwa kuteua shule tisa (9) na hivyo basi kuteua walimu tisa (9) ambao walishiriki katika utafiti huu.

# 2.4 Mbinu za Kukusanya Data

- **2.4.1 Usaili**
- Mtafiti alitumia mbinu hii kuwasaili walimu wanaofundisha Kiswahili katika kidato cha tatu katika eneo la Teso Kaskazini. Mbinu hii ilitumiwa kwa sababu iliwezesha utafiti huu kuwa na data za kutosha.
- **2.4.2 Uchunzaji**
- Mbinu hii ilitumiwa katika utafiti kuchunza stakabadhi za walimu kama vile andalio la somo, maazimio ya kazi na hifadhi za kazi ili kuthibitisha tu mbinu walizozitumia walimu kufundishia ushairi.

# 2.4.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

- Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na uchunzaji. Data iliainishwa kwa misingi ya malengo ya utafiti.
- Data zilizopatikana kwa kutumia mbinu ya usaili na uchunzaji na ambazo zilikuwa ni za kimaelezo, zilichanganuliwa kwa kutumia maelezo na mifano; maelezo kuhusu namna data hizo zilivyopatikana yalitolewa. Mifano iliambatishwa kwa maelezo kuhusu data zilizokusanywa kutoka kwa watafitiwa.
- Data za kitakwimu zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kukokoteza na kisha kuwasilishwa kwa njia ya majedwali.

# 3.0 Matokeo ya Utafiti

## 3.1 Namna Tamthilia Inavyotumiwa Kufundisha Mtindo Katika Ushairi

- Watafitiwa hawa walisema kwamba ndani mwa tamthilia kulikuwa na nyimbo ambazo zilikuwa na mtindo, hivyo basi mwalimu anapofundisha mtindo wa tamthilia anakuwa katika nafasi nzuri pia ya kufundisha mtindo wa nyimbo kwa wakati uo huo. Utafiti katika tamthilia ya Kifo Kisimani pia uliafikiana na maelezo ya watafitiwa.
- Watafitiwa hawa waliposailiwa walieleza kuwa tamthilia ilikuwa na mashairi huru ambayo yalikuwa na mtindo; hii ina maana kuwa mtindo wa ushairi ungefundishwa wakati mwalimu anapofundisha tamthilia. Maelezo yao yaliafikiana na utafiti katika tamthilia ya Mstahiki Meya.
- Watafitiwa walieleza kwamba tamthilia ilikuwa katika nafasi nzuri ya kutumiwa kufundishia mtindo katika mashairi ya arudhi. Utafiti ulirejelea tamthilia ya Kigogo kwa ajili ya kupata mfano wa shairi la arudhi lililokuwa na mtindo.

# 3.2 Matumizi ya Tamthilia Katika Ufundishaji wa Muundo wa Ushairi

- Watafitiwa walisema kwamba mwalimu anapofundisha mtindo katika ushairi anaweza kutumia tamthilia ili kuwabainishia wanafunzi namna muundo ulivyotumika katika utanzu wa ushairi. Maelezo yao yaliafiki utafiti katika tamthilia ya Kigogo.
- Watafitiwa walisema kuwa mashairi huru yalibainika katika tamthilia za Kiswahili na hivyo basi mwalimu alikuwa na uwezo wa kutumia tamthilia kufundishia muundo wa mashairi hayo huru. Maelezo yao watafitiwa yaliafikiana na utafiti katika tamthilia ya Mstahiki Meya.
- Wasailiwa walieleza kuwa muundo katika utanzu wa ushairi unaweza kufundishwa kwa kutumia tamthilia. Hii ni kwa sababu tamthilia ilikuwa na mashairi ya arudhi ambayo yalidhihirisha muundo wa ushairi. Maelezo yao watafitiwa yaliafikiana na utafiti katika tamthilia ya Kigogo.

# 3.3 Namna Tamthilia Inavyotumika Kufundisha Maudhui Katika Ushairi

- Watafitiwa walisema kwamba tamthilia inaweza kutumika kufundishia maudhui katika nyimbo. Maudhui yalipatikana katika nyimbo zilizowekwa katika tamthilia. Maelezo yao watafitiwa yaliafikiana na utafiti katika tamthilia ya Kigogo.
- Wasailiwa walieleza kuwa tamthilia inaweza kutumiwa kufundishia maudhui katika mashairi huru yanayobainika katika tamthilia husika. Maelezo yao yaliafikiana na utafiti katika tamthilia ya Mstahiki Meya.
- Watafitiwa walieleza kuwa maudhui katika mashairi ya arudhi yalipatikana katika tamthilia. Maudhui yaliyopatikana katika mashairi ya arudhi yaliyokuwa ndani mwa tamthilia yangefundishwa kwa pamoja na hivyo basi kueleweka sawasawa. Maelezo haya yaliafikiana na utafiti katika tamthilia ya Kigogo.

# 4.0 Hitimisho

- Utafiti huu ulihusu namna tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha ushairi katika shule za upili nchini Kenya kwa kuzingatia malengo matatu mahususi ambayo ni: kueleza namna tamthilia inavyotumiwa kufundisha mtindo katika ushairi, kubainisha matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa muundo wa ushairi na kuonyesha namna tamthilia inavyotumiwa kufundisha maudhui katika ushairi.

# 5.0 Mapendekezo

Mapendekezo ya utafiti huu ni kuwa:

- Usetaji katika ufundishaji na ujifunzaji uweze kutiliwa maanani na walimu wanapofundisha Kiswahili.
- Kando na tamthilia na ushairi, tanzu zingine za fasihi zionyeshe namna zinavyoweza kutumiwa kwa pamoja wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.
- Tafiti zionyeshe umuhimu wa ufundishaji wa tanzu mbili kwa pamoja.

Shukrani!